SUMAIT University Journal (SUJ)
ISSN (2507-7864)
Issue No: 11 (December 2022)

# CHANGAMOTO ZA ISTILAHI ZA KISWAHILI ZATEHAMA KWA JAMIILUGHA YA WASWAHILI

Ulfat Abdull-azizi Ibrahim
*madammullu@gmail.com*

*Department of Linguistics,*
*Abdulrahman Al-Sumait University, Zanzaibar,*
*E-mail address:*

*Received: January 2022, Accepted: April 2022, Published December 2022*
*© SUMAIT University Journal 2022*

**Abstract:**
*This article aims to explore the various challenges posed by ICT terminology in the Swahili community of Zanzibaris. Information and Communication Technology has brought about significant changes and developments in our communities. Development in any society goes hand in hand with the efforts that community members themselves make to cope with the changes taking place in their community. The same to the Swahili language community which at this moment, is in the development of science and technology. Confirming this point Kin'gei in Simala and colleagues, (2008: 221) stated: "The Swahili language has begun to be used in a number of academic and scientific fields thus creating an urgent need for new terminology to express concepts in those fields. Examples of these new areas of usage are Information and Communication Technology ... ". These developments have made the language community one of the most important users of information and communication technology. Since the main role of language is communication, this has made language the lifeblood of the development of information and communication technology (ICT). This article explores the challenges by using interview techniques conducted to various computer users and social networks. This article identified some of the challenges that users face, including the complexity of the terminology. In this article the author proposes a variety of factors including the involvement of language users and professionals from various areas in terminology development to protect and preserve social ideologies.*

## IKISIRI

*Makala haya yamelenga kuchunguza changamoto mbalimbali zinazotokana na istilahi za TEHAMA katika jamii ya Waswahili ya Wazanzibari. Teknolojia ya habari na mawasiliano imeleta mabadiliko na maendeleo makubwa katika jamii zetu. Maendeleo katika jamii yoyote ile huenda sambamba na jitihada ambazo kwazo wanajamii wenyewe huzifanya ili kukabiliana na mabadiliko yanayotokea katika jamii yao. Vivyo hivyo kwa jamiilugha ya Waswahili ambayo kwa zama hizi imo katika maendeleo ya sayansi na teknolojia. Akithibitisha hoja hiyo Kin'gei (2008:221) amesema: "Lugha ya Kiswahili imeanza kutumika katika nyanja kadhaa za kitaaluma na kisayansi na hivyo kuzua haja ya dharura ya kuwapo kwa istilahi mpya kuelezea dhana katika nyanja hizo. Mfano wa maeneo hayo mapya ya matumizi ni kama vile Teknolojia ya Habari na Mawasiliano…". Maendeleo hayo yameifanya jamiilugha hii kuwa ni miongoni mwa watumiaji wa teknolojia ya habari na mawasiliano. Kwa vile dhima kuu ya lugha ni mawasiliano, hii imeifanya lugha kuwa ndio damu katika maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA). Makala haya yametumia mbinu ya usaili kwa kuwahoji watumiaji mbalimbali wa kompyuta na mitandao ya kijamii. Makala yamebaini miongoni mwa changamoto zilizojitokeza kwa watumiaji ni pamoja na ugumu wa*

*kutoeleweka kwa istilahi hizo na kusababisha kutokutumika. Katika makala haya ili kuikabili changamoto hii ya kutokukubalika kwa msamiati huu wa TEHAMA, mwandishi anapendekeza mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ushirikishwaji wa watumiaji wa lugha na wataalamu kutoka maeneo ya jamiiilugha ya Waswahili mbalimbali katika uundaji istilahi ili kulinda na kuchunga itikeli za jamii ya Waswahili?.*

**Keywords:** ***Istilahi, jamiilugha, Kilinux na TEHAMA***

## 1.0 Utangulizi

Lugha ya Kiswahili imekumbana na mabadiliko ya kiulimwengu ya kutoka katika mfumo wa analojia kwenda dijiti, hii inatokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia yalivyoingia katika jamii za Waswahilizetu. Wataalamu mbalimbali wameeleza juu ya hatua za maendeleo zilizofikiwa na lugha ya Kiswahili.Akieleza kuhusu upeo wa lugha ya Kiswahili Momanyi (2016), anaeleza " ni ukweli usiopingika kuwa lugha hii (Kiswahili) sasa imekuwa mojawapo ya lugha za teknolojia ya mawasiliano na inatambulika kama asasi inayoweza kujenga na kuimarisha utangamano mzuri baina ya mataifa

Maelezo haya ya Momanyo yanadokeza kwamba kuna istilahi za TEHAMA zilizoundwa kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Kwa maoni ya waandishi wa makala haya kama wanaisimujamii tumeamua kufanya tathmini kuhusu istilahi hizo na kuzichunguza ili kubaini changamoto ambazo jamii inakumbana nazo katika kutumia istilahi hizo katika maisha yao ya kijamii ya kila siku.

Kwa kawaida istilahi za Kiswahili huundwa na asasi na taasisi zenye mamlaka ya kisheria kama vile Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA), Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) zikishirikiana na Taasisi za elimu ya juu. Kupitia vyombo hivyo rasmi kunakuwa na miradi mbalimbali ambayo imejishughulisha na uundaji wa istilahi za TEHAMA.

Moja kati ya miradi hiyo ni mradi wa Kilinux. Aidha, moja kati ya makusudio na jitihada za mradi huu wa uundaji wa istilahi za programu huria (Kilinux) ni kuingiza Kiswahili katika TEHAMA. (Taz:http://www.kilinux.udsm.ac.tz)

Istilahi zilizoundwa ni nyingi na zimeshaingizwa katika programu mbalimbali za kompyuta ili watumiaji waweze kutumia vifaa hivyo kwa urahisi.

Makala haya yamechunguza kuhusu changamoto za istilahi hizo na kuzigawa katika sehemu sita zifuatazo: sehemu ya kwanza ni utangulizi,pili ni maelezo kuhusu dhana mbalimbali zilizotumika katika makala haya, tatu, mbinu zilizotumika katika uundaji wa istilahi za Kiswahili za TEHAMA katika mradi wa Kilinux, nne, changamoto za istilahi za TEHAMA. Sehemu ya tano ni mapendekezo na sehemu ya mwisho ni hitimisho.

## A. UFAFANUZI WA DHANA MBALIMBALI ZILIZOTUMIKA KATIKA MAKALA HAYA

### Dhana ya Jamiilugha

Kwa mujibu wa Mekacha (2011) ameelezea kwamba, Jamiilugha ni watumiaji wa lugha wanaoishi katika eneo moja ambao hubainishwa kwa mahusiano yao ya kuendelea kutumia aina fulani ya lugha tofauti na watumiaji wengine wa lugha hiyo hiyo. Fasili hii imejikita zaidi katika msingi wa kutumia lugha, ambapo inaaminika kwamba lugha hutumika kama nembo ya jamii fulani ambapo watu wanatoka au wanapopatikana.

### Dhana ya TEHAMA

TEHAMA ni finyanzo inayotokana na maneno matatu yenye maana ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. TEHAMA ni dhana ya jumla inayotilia mkazo mawasiliano ya pamoja na mwingiliano wa mifumo ya mawasiliano (mikonga ya simu na mawimbi upepo), ujenzi wa mifumo imara ya usimamizi na mifumo ya sauti-picha katika teknolojia ya habari ya kisasa. TEHAMA inajumuisha mahitaji yote ya kiufundi kuwezesha habari na kusaidia mawasiliano. Pia, TEHAMA kwa ujumla wake hurejelea mifumo yote ya kiteknolojia inayotumika kutengeneza, kuhifadhi, kuchakata na kutumia habari katika mifumo yake tofauti tofauti ambayo huwezesha, kurahisisha mawasiliano. TEHAMA inajumuisha matumizi ya simu, vyombo vya kurusha matangazo/habari, aina zote za kuchakata na kurusha sauti na picha na miundo ya mitandao ya usimamizi na ufuatiliaji.

TEHAMA ni nyanja mpya katika Ulimwengu wa sayansi na teknolojia, na si tu kwa upande wa lugha ya Kiswahili kama wengi tunavyodhani. Hii ni kwa sababu kadiri siku zinavyosonga mbele teknolojia mpya huzaliwa, ikiwa ni pamoja na kuzalisha vifaa, vyombo na vitu vipya vya kurahisisha au kuboresha maisha ya jamii. Hapo basi lugha ya Kiswahili ndipo ilipokuwa na uhitaji wa Istilahi, ili kuiwezesha lugha hii kukidhi mahitaji ya watumiaji wake. Mradi wa Kilinux ni mmoja kati ya miradi iliyojitolea kuwasaidia wanajamiilugha ya Waswahili waweze kutumia mtandao kwa njia rahisi.

### Dhana ya Kilinux na Historia yake kwa Ufupi

Kilinux ni Mradi wa kuingiza Kiswahili katika Programu Huria. Mradi huu ulianzishwa mwaka 2003 na Idara ya Sayansi ya Kompyuta – Chuo Kikuu cha Dar es salaam kwa kushirikiana na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) - Chuo Kikuu cha Dar es salaam na Chuo Kikuu Kishiriki cha Uhandisi na Teknolojia. Lengo kubwa la mradi huu ni kukifanya Kiswahili kitumike katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Timu ya Kilinux imejanibisha na kutoa mazao mawili yanayoitwa *Jambo Mozilla Firef*ox 1.0.3 na *Jambo Open Office.org* 1.0.3.

Lengo hasa la mradi huu ni kuhamasisha watumiaji wa Kiswahili katika utumiaji wa progaramu huria pamoja na manufaa yake. Aidha, uingizaji wa programu za kompyuta katika Kiswahili, utapunguza kwa kiasi kikubwa muda wa mafunzo unaohitajika kumwezesha mwanafunzi kutumia kompyuta kwa vile tayari mwanafunzi atakuwa anaelewa vyema lugha ya kujifunzia.

Mnamo mwaka 2004 mradi wa Kilinux ulifanikiwa kuunda istilahi 1500 za Kiswahili ambazo istilahi 900 ni juzuu ya kwanza kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya kompyuta. Pia tarehe 15 Juni 2006, mradi huu ulitangaza kujanibishwa kwa kivinjari (*web browser*) cha *mozilla firefox*(http://www.kilinux.udsm.ac.tz/kblog_sw/archives/cat_2.html).

**Dhana ya Istilahi**

Dhana ya istilahi ni dhana ambayo imejikita katika uwanja maalum wa maarifa. Kwa kawaida kila uga huwa na msamiati wake ambayo hutumiwa kwa ajili ya kuwakilisha dhana fulani mahususi. Hivyo basi istilahi inatokana na msamiati ambao ni mahususi katika fani au uwanja maalumu.
Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili sanifu (1981), imeeleza kwamba " Istilahi ni neno litumikalo kwa ufupi wa maneno mengi ya kiufundi kufuatana na elimu fulani kama vile sayansi, siasa, uchumi n.k ". Naye Mkude (2004) ameeleza dhana ya istilahi kwamba ni msamiati uliosukwa kimkakati na kuratibiwa kwa nia ya kuashiria dhana teule za taaluma fulani.

Kutokana na mawazo ya wataalamu tajwa hapo juu, tunaweza kusema kwamba istilahi ni maneno maalum ambayo hutumika katika fani fulani kuwakilisha dhana katika fani hiyo. Yawezekana kuwa istilahi likawa ni neno la kawaida, lakini neno hilo limekuwa istilahi kwa sababu ya matumizi yake katika uwanja maalumu. Aidha, kila uga huwa na istilahi zake ambazo hubeba dhana muhimu zinazotumika katika uga huo. Maana yake huwa si nje ya taaluma hiyo na hufahamika tu na wazungumzaji pamoja na watumiaji wa lugha hiyo katika uwanja huo maalum. Kwa mfano msamiati unaotumika katika lughawiya/isimu, fasihi, teknolojia ya habari na mawasiliano na kadhalika ni maalumu na hutumiwa na kueleweka tu na watumiaji wahusika na nyanja husika. Kwa mfano; neno '*pakua*' ni neno la kawaida linalowakilisha kitendo cha kutoa kitu kwenye sehemu fulani na kuingiza katika sehemu nyingine, kama vile kupakuwa chakula kutoka katika sufuria na kukiweka katika sahani au chombo chochote kwa ajili ya kuliwa. Matumizi katika mazingira ya kompyuta neno '*pakua*' inaelezea kutoa kitu katika sehemu moja kwenda nyingine kwa namna maalum. Kupakua katika kompyuta ni kutoa kitu, ikiwa ni matini au hata picha kutoka katika mtandao.

Hivyo basi, nikusema kwamba si kila msamiati ni istilahi bali msamiati huwa istilahi pale unapotumika katika nyanja fulani mahususi.

Nchini Tanzania jukumu la kuunda istilahi limetwikwa kwenye vyombo rasmi kama Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA), Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaa, Taasisi ya Elimu, Wizara ya Elimu, idara za Fasihi, Lugha na Isimu za Vyuo Vikuu mbalimbali. (Kevogo, 2016)

Kwa mujibu wa BAKITA kuna kanuni maalumu ambazo hazinabudi kufuatwa katika kuunda istilahi. Kanuni hizo hazina tofauti na zile zilizoorodheshwa na shirika la viwango la kimataifa, ambalo miongoni mwa kazi zake ni kuratibu na kusimamia uendelezaji wa istilahi kimataifa. Nazo ni hizi zifuatazo:

(1) Istilahi ziundwe baada ya kupata dhana iliyoelezwa kwa ukamilifu na wazi.

(2) Istilahi ziwe fupi kadiri iwezekanavyo lakini zenye kueleweka.

(3) Istilahi ziundwe kwa kufuata mofolojia ya kawaida ya lugha.

(4) Istilahi ziundwe kwa njia ambayo itakuwa rahisi kuunda istilahi nyingine kwa mnyumbuliko.

(5) Uundaji wa istilahi kwa kupanua maana ya neno uepukwe hasa iwapo nyanja zinazotumia maneno hayo zinakaribiana, ili kuepusha utata. Kwa hiyo mfumko wa sinonimia au homonimia (visawe) hauna budi kuepukwa ili watumiaji wasikanganyikiwe.

Lugha mbili zinapohusika kanuni zifuatazo zizingatiwe:

(1) Uundaji wa istilahi kwa njia ya kukopa (kutohoa) maneno ya lugha nyingine uzingatie kuchukua maneno kama yalivyo katika lugha ya asili na kufanya marekebisho machache tu ili kulingana na sarufi na matamshi ya lugha pokezi. Njia hii, imedhihirika katika uundaji wa baadhi ya istilahi za TEHAMA Kwa mfano :

| | |
|---|---|
| Adapta | (adopter) |
| Menyu | (menu) |
| Dijiti | (digit), n.k. |

(2) Uundaji wa istilahi kwa kutumia Kigiriki na Kilatini uendelezwe ili kuzingatia uwakilishi sahihi wa dhana hasa za sayansi na pia kupunguza kishawishi cha kupendelea kutumia baadhi tu ya lugha zinazotumika ulimwenguni hivi sasa.

Katika uzoefu wa kusanifu istilahi, BAKITA imekuwa ikizingatia pia kanuni za nyongeza ili kupata ufanisi zaidi kwa kutilia maanani jamii ya watumiaji wa Kiswahili na utamaduni wake. Kubwa kati ya kanuni hizo za nyongeza ni:

- **Istilahi ziepuke utusani**; yaani zisiundwe kwa maneno ambayo tayari yanaeleweka kwamba ni matusi kwa watumiaji.
- **Istilahi ziwe angavu;** yaani istilahi ziweze kudokeza dhana liliyokusudiwa kwa kina na usahihi kadiri iwezekanavyo.
- **Istilahi ziwe na ulinganifu wa mtiririko ulio katika dhana za kikoa kimoja**; Katika hili ni muhimu kwa wasanifishaji kukumbuka kwamba istilahi hazikai pekee, istilahi zilizozoeleka

au kukomaa kutokana na kutumika kwa muda mrefu zisibadilishwe. Kanuni hii ni muhimu sana katika ukubalifu wa istilahi zinazoundwa.

Tajiriba ya BAKITA imeonyesha kuwa ni vigumu kwa istilahi mpya kukubaliwa na kushamiri pale ambapo tayari kulikuwa na Istilahi zilizokuwa zikitumika, hasa zile za muda mrefu. Kwa mfano neno *Ovataimu* (overtime) lililokuwa limezoeleka kwa muda mrefu limeendelea kutumika badala ya neno *ajari*. Vivyo hivyo neno *mdai* (creditor) limeendelea kutumika badala ya neno *mwia*. Maneno yote mawili ni ya siku nyingi lakini neno *mdai* limezagaa zaidi katika matumizi kuliko neno *mwia*. (Mtesigwa 2004:11-22)

Aidha, istilahi za TEHAMA zimeundwa kwa kuzingatia kanuni. Kahigi (2007) amethibitisha hilo kwa kusema, istilahi za TEHAMA ambazo zimeundwa kwa kuzingatia kanuni na mbinu ambazo zilitoka katika machapisho ambayo yanakubaliana na maelekezo ya Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO). Machapisho hayo ni kama vile Terminology Manual (Feber. H (1984)), na J.C Sager (1990) A practical course in Terminology Processing.

Kwa vile kazi hii ilijikita katika kuchunguza Istilahi za TEHAMA zilizoundwa chini ya mradi wa programu huria ya Kilinux, hivyo basi hapana budi kutalii kwa ufupi mbinu mbalimbali ambazo zimebainika kutumika katika uundaji wa Istilahi hizo.

#### B. MBINU ZILIZOTUMIKA KATIKA UUNDAJI WA ISTILAHI ZA KISWAHILI ZA TEHAMA KATIKA MRADI WA KILINUX;

Kwa mujibu wa Malagira, (2010), ameelezea juu ya mbinu kadhaa zifuatazo zilizotumika katika kupata istilahi za TEHAMA katika programu ya Kilinux:

**Unyambulishi:**

Katika mbinu hii kitenzi kinaweza kugeuzwa kikawa nomino au kivumishi kinaweza kugeuzwa kikawa kitenzi au nomino. Mbinu hii imetumika kwa kiasi kikubwa, mifano ifuatayo hudhihirisha matumizi ya mbinu hii.

Accessing > ufikio (viambishi u-i-o vimeambatishwa katika shina fika).

Accsess > fikio (viambishi i-o vimenyambulishwa katika shina fika)

**Mwambatano:**

Hii ni njia inayotumika kwa kuambatanisha maneno mawili au zaidi. Katika Kilinux kuna istilahi zenye mwambatano wa maneno mawili na mwambatano wa maneno matatu.

Mifano ifuatayo inadhihirisha matumizi ya mbinu hii:

Add-on help > msaada nyongeza (yameambatishwa maneno msaada na nyongeza).

Alphabet text character > kiwambo alfabeti (kiwambo + alfabeti).

Aperture value > thamani upenyo (thamani + upenyo)

**Muungano:**

Hii ni mbinu ya kuunganisha maneno mawili au zaidi ili kupata neno moja; mbinu hii pia imetumika kuunda istilahi za Kiswahili katika Kilinux. Mifano ifuatayo inabainisha kutumika kwa mbinu hii:

Anonymity > ufichojina (uficho + jina).

Arccosine > kosinitao (kosini + tao).

Backslashes > mkwajunyuma (mkwaju + nyuma).

**Ukopaji:**

Njia hii pia imetumika kuunda istilahi za Kiswahili katika Kilinux. Mifano ifuatayo inaonyesha kutumika kwa mbinu hii.

Account > akaunti

Adapter > adapta

Ampersand > ampasendi

**Tafsiri mkopo:**

Mbinu nyingine iliyotumika kwa kiasi kikubwa katika uundaji wa istilahi za Kiswahili katika Kilinux ni mbinu ya tafsiri mkopo (tafsiri sisisi). Tafsiri mkopo ni tafsiri ya moja kwa moja kutoka lugha chanzi. Mifano ifuatayo inathibitisha matumizi ya mbinu hii katika uundaji wa istilahi za Kiswahili katika Kilinux.

Actions menu > menyu vitendo.

Address book > kitabu cha anwani.

Alert me > nitahadharishe.

**Ufupishaji:**

Mbinu hii pia imetumika katika kuunda istilahi za Kiswahili katika Kilinux; hii ni mbinu inayotumika kufinyanza fungu la maneno na kupata neno moja. Mifano ifuatayo huonyesha matumizi ya mbinu hii:

Alt (alternate) > Kbdl (kibadala)

BSS (Bulletin Board Service) > HUM (Huduma za Ubao wa Matangazo)

Ctrl (ontrol) > Kdbt (kidhibiti)

**Uhulutishi:**

Ni mbinu pia liyotumika katika uundaji wa istilahi za Kiswahili katika Kilinux, mbinu hii hutumika katika uundaji wa istilahi kwa kuunganisha sehemu za maneno na kuunda neno moja. Mbinu hii imetumika kwa kiasi kidogo sana, rejea mifano ifuatayo:

Bitmap > taswidoti ((taswi) ra + doti)

Multimedia > medianuwai ((medi) a + anuwai)

Mbinu nyingine iliyotumika katika uundaji wa istilahi za Kiswahili katika Kilinux lakini kwa kiasi kidogo sana ni ile mbinu ya upanuzi wa maana za maneno, upanuzi wa maana za maneno ni kuongezea maana maalumu za kiistilahi katika maneno ya Kiswahili.

Mfano: mouse > puku

Puku kwa maana ya kawaida ni panya pori lakini hapa limepewa dhana mahususi katika kompyuta kwa maana ya kifaa kinachotumika katika utumiaji wa kompyuta.

**Utemaji (clipping):**

Mbinu hii pia iliyojitokeza kwa kiasi kidogo sana, kwa kutumia mbinu hii istilahi huundwa kwa kukata sehemu ya neno na sehemu ya neno itakayobaki hutumika kama istilahi. Mfano: key (on keyboard) > kibonye (kutoka neno bonyeza na kuongeza kiambishi cha ngeli ya saba ki-).

Kwa hiyo hizi ndizo baadhi ya mbinu zilizobainika kutumika katika uundaji wa istilahi za Kiswahili zilizoingizwa katika mfumo wa kompyuta wa Kilinux. Licha ya kubainika mbinu mbalimbali za uundaji wa istilahi hizo, imebainika kwamba kuna changamoto mbalimbali ambazo watumiaji wa istilahi hizo wanakumbana nazo katika kuzitumia istilahi hizo na kusababisha kurudisha nyuma jitihada za waundaji istilahi katika jamiilugha ya Waswahili.

## C. CHANGAMOTO ZA ISTILAHI ZA TEHAMA

Baada ya istilahi nyingi kuundwa, kama lilivyokuwa lengo la waundaji wa istilahi kuwasaidia watumiaji kuweza kutumia teknolojia kwa urahisi. Changamoto kadhaa zimejitokeza kwa watumiaji wa istilahi hizo, nazo ni hizi zifuatazo:

Kutokujulikana kwa istilahi za TEHAMA.Wanajamiilugha wanahitaji uelewa wa kutosha juu ya zao lolote linalotengenezwa kwa ajili yao. Jamiilugha imeonekana kutokuwa na taarifa juu ya istilahi ambazo zimeundwa. Asilimia kubwa ya jamiilugha ya Waswahili hawajui lugha za Kimagharibi hususan Kiingereza. Kama alivyoeleza Rubagumya (1989) kuwa ni wastani wa 15% tu ya watu wanaoishi Tanzania wana uwezo wa kuzungumza Kingereza.

Istilahi zimeundwa lengo ni kuwasaidia hususan wasiojua Kiingereza waweze kutumia mtandao kwani maarifa haya awali yamekuja kwa lugha za Kimagharibi. Jambo la kushangaza ni pale inapogundulika ya kwamba, mbali ya watu walioko kijijini ambao asilimia kubwa hawajui lugha ya Kiingereza, hata wale walioko katika Taasisi za elimu ya juu ambao wengi wao ni watumiaji mtandao, nao hawajui kwamba kuna istilahi zilizoundwa ili ziwasaidie wao katika kutumia mtandao.

**Kutokutumika kwa Istilahi za TEHAMA.** Matarajio yetu wanajamiilugha ni kutumia mtandao kwa wepesi. Kutokana na hoja niliyoitanguliza ya kutokujulikana kwa istilahi hizo, basi hata kiwango cha matumizi si cha kuridhisha. Hii ni kwa sababu ni wachache wanaojua kwamba kuna istilahi za Kiswahili za TEHAMA. Istilahi zimo katika mifumo ya teknolojia kupitia huduma mbalimbali kama vile simu za kiganjani, mashine za Bank za kutolea pesa,(ATM), na kwenye programu mbalimbali kama vile google n.k. Utafiti huu unaonesha kwamba watu wanapotumia huduma hizo hupendelea zaidi kutumia lugha ya Kiingereza kuliko Kiswahili. Kwa kisingizio cha ugumu wa maneno na mazoea ya kutumia Kiingereza. Wanajamiilugha wanaotumia Kiingereza katika huduma hizo wamejigawa katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni wale wenye uelewa wa lugha ya Kiingereza, na wameshazoea kutumia lugha hiyo. Kundi la pili ni wale wasio na uelewa wa lugha ya Kiingerza bali hutumia huduma hizo kwa lugha ya Kiingereza kutokana na kukariri zile hatua zinazopitiwa katika kupata huduma fulani, au kwa kutumia alama kama vile picha hususan katika simu za viganjani.

**Kutokueleweka kwa dhana zilizowakilishwa na istilahi za TEHAMA.** Jamiilugha inalalamika juu ya ugumu wanaoupata katika kuelewa kilichokusudiwa. Lugha iliyotumika sio nyepesi au ya kawaida ambayo ni rahisi kueleweka. Kwa mfano:

*absolute* - *kenyekenye*
*archiving* - *ujalidi*
*home directory* - *saraka kaya*
*crop* - *pogoa*
*clients* - *koteja*
*charset* - *setikibambo*

wengi watakubaliana nami kwamba haya maarifa tumeyapata kutoka katika jamii nyingine. Hizi dhana tumehamisha kutoka katika jamiilugha ngeni iliyoanza nayo. Hivyo basi wakati tunapohamisha dhana tujaribu kufikiria na msamiati ambao utawakilisha dhana hizo. Iwapo kwa lugha ya kawaida utakosekana si aula kutumia lugha za Kibantu. Makala haya hayana lengo la kuidharau lugha yetu, la hasha! Lengo ni kurahisisha mawasiliano. Ni vyema kukopa msamiati na kuuweka kwa mujibu wa sarufi ya lugha ya Kiswahili ili wanaotumia waweze kuelewa dhana kwa urahisi.

**Dhana moja kuwa na istilahi zaidi ya moja.** Changamoto nyingine tuliyoibaini ni istilahi moja kurejelewa kwa istilahi zaidi ya moja. Hii inaleta mkanganyiko kwa watumiaji. Utofauti huu unaweza kupoteza hamu na kasi ya kutumia istilahi. Akielezea juu ya mkanganyiko huo Momanyi (2016) ameelezea utofauti wa istilahi zilizoundwa chini ya programu ya *microsoft* mnamo mwaka 2004 na zile zilizomo katika kamusi ya kompyuta na teknolojia ya lugha ya Kiputiputi (2011). Amebainisha baadhi ya istilahi kama vile neno "akibisha" Kiputiputi (2011) amelipa maana ya kuhifadhi data ya ziada kwa upande wa Jopo la *Microsoft* lilitoa maana ya *' hifadhi'*

Tatizo hilo pia limejitokeza katika istilahi zilizoundwa na jopo la Kilinux na kamusi sanifu ya kompyuta na teknolojia ya lugha ya Kiputiputi (2011). Kwa mfano neno Kompyuta aina ya " *laptop*" Kiputiputi (2011) amelipa maana ya ' k*ompyuta za pajani'/'kompyuta bebe'/'kompyuta jota'*. Jopo la Kilinux lilitoa maana ya 'kompyuta ya mkononi'. Mkanganyiko wa aina hii ndio huleta changamoto kwa watumiaji

**D. Mapendekezo**

Tatizo la kutokujulikana kwa istilahi za TEHAMA linaweza kutatuka iwapo waundaji wa istilahi baada ya kuunda watazisambaza kwa watumiaji kupitia Taasisi husika kama vile vyombo vya habari pamoja na mitandao ya kijamii kuhakikisha istilahi walizoziunda zinajulikana na wengi.

Ili istilahi zinazoundwa ziweze kutumiwa waunda istilahi hawanabudi kuzifanyia kazi zile ambazo zimeshazoeleka. Kwa namna nyingine ni kusema mbinu ya ukopaji inaweza kusaidia kuondoa changamoto hii. Iwapo mtumiaji amezoea kutumia neno *Disc* akakuta neno la Kiswahili ni *Diski* na maneno mengine mithili ya hayo, watumiaji hawataona ugumu kutumia istilahi hizo.

Aidha, kutokueleweka kwa dhana ni kikwazo kikubwa kwa watumiaji. Waundaji wa istilahi wazingatie kanuni za uundaji Istilahi. Tukirejelea moja ya kanuni zilizobainishwa na BAKITA (weshatajwa) wanaeleza " undaji wa istilahi kwa kutumia Kigiriki na Kilatini uendelezwe ili kuzingatiauwakilishi sahihi wa dhana hasa za sayansi...". vievile kanuni nyingine inasisitiza kwamba"***Istilahi ziwe angavu,***yaani istilahi iweze kudokeza dhana iliyokusudiwa kwa kina na usahihi kadiri iwezekanavyo. Kutokuzingatiwa kwa kanuni hizo kunasababisha matatizo kwa watumiaji. Hatimaye lengo lilokusudiwa linashindwa kufikiwa.

Kuhusu tatizo la dhana moja kuwa na istilahi zaidi yamoja, ni vyema kabla kuunda istilahi mpya turudi katika jamii kuchunguza kama kuna istilahi zilizokwisha tangulia ili tuepushe mkanganyiko huu. Vilevile kuwepo na chombo maalumu ambacho waundaji wa istilahi wote lazima wapitie hapo kabla ya istilahi hizo kuwafikia walengwa. Chombo/ Tasisi hiyo iwashirikishe wataalamu wa lugha, wataalamu wa istilahi, na watumiaji wa lugha.

### E. Hitimisho

Makala haya yamebainisha changamoto mbalimbali za istilahi za TEHAMA ambazo wanajamiilugha ya Waswahili wanakumbana nazo katika matumizi yao ya TEHAMA. Hoja zilizojitokeza ni kwamba baadhi ya watu katika jamiilugha ya Waswahili hawajui kwamba kuna istilahi zilizoundwa kwa ajili ya kuwasaidia waweze kutumia TEHAMA kwa urahisi, pia ugumu wa istilahi ni tatizo jingine linalorudisha nyuma maendeleo ya lugha kwani wanashindwa kuzitumia kwa sababu ya kutozielewa. Aidha, utofauti wa istilahi miongoni mwa waundaji wa istilahi unasababisha mkanganyiko wa istilahi ipi ni sahihi kwa dhana husika. Pamoja na changamoto hizo makala haya yamependekeza njia zitakazosaidia kupunguza ama kuondosha kabisa changamoto hizo ikiwa na pamoja kuzingatia mbinu za uundaji istilahi, kuchagua msamiati ambao utakuwa ni rahisi kueleweka. Vilevile kuwe na chombo maalumu ambacho kitawashirikisha wataalamu wa lugha, waundaji wa istilahi pamoja watumiaji wa istilahi. Pia, istilahi zote zinazoundwa lazima zipitie hapo ili kuepusha kujirudia rudia kwa istilahi tofauti zenye kuwakilisha dhana moja. Makala haya yanaweza kutoa mchango kwa waundaji wa istilahi na kuleta mabadiliko katika maendeleo ya lugha ya Kiswahili katika ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia.

### MAREJEO

- Kahigi, K.K. (2007) Ujanibishaji wa Office 2003 na Windows XP kwa Kiswahili Sanifu katika Kioo cha Lugha, Jarida la Kiswahili na Fasihi. Juzuu 5: Idara ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Oar es Salaam.
- Kiputiputi, O.M.(2011). Kamusi Sanifu ya Kompyuta. Dar es salaam: university of Dar es salaam. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili ( TATAKI)
- Malagira, A. (2010). Mbinu zilizotumika katika uundaji wa Istilahi za Kiswahili zilizoingizwa katika mifumo ya mawasiliano ya Kompyuta wa Linux. Chuo Kikuu cha Dare es Salaam.
- Mekacha (2011). Isimujamii:nadharia na muktadha wa Kiswahili.Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
- Momanyi, Clara (2016). 'Chachawizo la Msamiati na istilahi za Kiswahili katika kukidhi mahitaji ya Kiutandawazi: Umuhimu wa Usanifishaji.Twaweza Communications Ltd.Nairobi, Kenya.

- Mkude, D. (2002). *Minority Language and Democratization Process in SADC Region:* The case of Tanzania.In talking freedom, ed. By Karsten Legere and Sandra Fitchat.Windhoek: Gamsberg Publishers.
- Mtesigwa, P. (2014). Uundaji wa Istilahi. Uzoevu wa Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA). Paper given at the Klnx workshop, 1-5 November 2004.
- Simala na wenzake (2008). *Nadharia katika taaluma ya Kiswahili na lugha za kiafrika*. Eldoret, Kenya: Moi University Press.
- Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) (1981) Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Nairobi, Dar es Salaam: Oxford University Press.
- University of Dar es Salaam (UDSM) and IT +46 (2004). The Kilinux Project, Department of Computer Science and the Institute of Swahili Research. http://www.it46.se/projects/SIDA_jambo.
- University of Dar es Salaam (UDSM) and IT +46 (2004), KlnX IT Glossary. http://www.it46.se/docs/development/sw_TZ_glossary_klnX_1.pdf
- http://www.appropedia.org/Teknohama